

## **COVID-19 na afya na salama za kazi – Biashara ndogo**

### **Kutathmini na kusimamia hatari**

COVID-19 imebadilisha njia sisi sote tunavyoishi na kufanya kazi. Lakini sekta ya biashara ndogo inaendelea.

Tathmini ya hatari ya afya na usalama wa kazi ya COVID-19 ni hatua muhimu kwa biashara ndogo, kutambua na kusimamia hatari kwako, kwa wafanyakazi wako, na wateja wako.

Unapofanya tathmini ya hatari, jiulize:

- Zipo hatari gani?
- Je! Ingeweza kusababisha shida gani kwa mtu, na ina uwezekano gani?
- Kiwango cha hatari ni nini?
- Je! Naweza kufanya nini kusimamia hatari?
- Je! Hatari hiyo itakaguliwa na kufuatiliwa jinsi gani, ili kuhakikisha kuwa hatua za kusimamia zinafaa na kuangalia kwa hatari mpya?

Usimamizi wa hatari unaendelea - hakikisha kutathmini hatari zozote mpya au zilizobadilika kutokana na COVID-19, kama hatari kutoka kwa uchokozi wa wateja, mahitaji ya kazi nyingi au kufanya kazi katika kutengwa.

Unapaswa kuzungumza na wafanyakazi wako. Pamoja mnaweza kutambua hatari na kufikiria jinsi ya kuzishughulikia.

Sote tuendeleza sekta ya biashara ndogo. Kwa habari zaidi, enda kwa tovuti - [safeworkaustralia.gov.au](https://safeworkaustralia.gov.au).

### **Umbali wa mwili**

Hatari ya kupatikana kwa COVID-19 huongezeka wakati wa kufanya kazi kwa kukaribiana na wengine. Ikiwezekana, fanya umbali wa mwili.

Fikiria:

- Kuandaa tena muundo wa mahali pa kazi.
- Kufanya mikutano ya usoni.
- Kupunguza idadi ya watu katika maeneo ya kawaida.
- Kusimamia foleni na nambari za wateja.



Na inapowezekana, acha muda kati ya miadi ili kupunguza mwingiliano wa mwili na hakikisha wafanyakazi wana zana yao au vifaa vyao.

Kwa miongozo maalum ya tasnia kuhusu COVID-19, kwenda kwenye [safeworkaustralia.gov.au](https://safeworkaustralia.gov.au).

### **Kusafisha mahali pako pa kazi**

COVID-19 huenea kupitia matone yanayotengenezwa wakati mtu aliyeambukizwa anapokohoa au kupiga chafya.

Watu wanaweza kupata COVID-19 kwa kugusa uso ambao una viini juu yake.

Hakikisha mahali pako pa kazi husafishwa angalau kila siku na sabuni na maji.

Mara tu uso ukiwa safi, unaweza kuu virusi.

Weka kipaumbele kusafisha nyuso ambazo zinaguswa mara nyingi.

Ikiwa una kesi ya COVID-19 kazini, sehemu yako ya kazi itahitaji kusafishwa kabisa pamoja na dawa ya kemikali kabla ya watu kuweza kurudi.

Kwa miongozo maalum ya tasnia kuhusu COVID-19, angalia kwenye [safeworkaustralia.gov.au](https://safeworkaustralia.gov.au).

### **Tovuti ya Safe Work Australia COVID-19**

Safe Work Australia imeunda mwongozo mpya ili kusaidia biashara ndogo kuelewa majukumu yao ya afya na usalama wa kazi, na kusimamia hatari inayotokana na COVID-19.

[safeworkaustralia.gov.au](https://safeworkaustralia.gov.au) ina habari juu ya mada kama jinsi ya kuvyofanya tathmini ya hatari, umbali wa mwili, usafi, vifaa vya kinga vya kibinafsi, afya ya akili, na kusafisha.

Tumia kifaa cha kuchuja yaliyomo ili kupata habari inayofaa kwa rahisi kwa biashara ndogo na tasnia yako, na pia rasilimali za vitendo, kama orodha za ukaguzi wa mahali pa kazi na mabango.

Kwa mwongozo maalum wa tasnia yako, angalia mtandaoni sasa - [safeworkaustralia.gov.au](https://safeworkaustralia.gov.au).